

Kuhifadhi watoto kutokana na ugonjwa wa TB

BCG na Mtoto wako

Mwendo wa kutopatwa na ugonjwa, njia ya usalama sana ya kuhifadhi mtoto wako.

DAWA LA BCG NA MTOTO WAKO

Ukurasa huu inahusika na dawa la BCG (Bacillus Calmette-Guerin) inayotolewa kumhifadhi mtoto wako kutokana na ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB).

Nini dawa la BCG?

Dawa la BCG linayo aina fulani ya vijimea vidogo (wadudu) vilivyodhoofika na kusababisha ugonjwa wa kifua kikuu. Kwa kuwa vimeshadhoofika, havitasababisha kifua kikuu, lakini vitamsaidia mtoto wako kujihifadhi (pasipo ugonjwa) kutokana na ugonjwa huo kama akishikwa na athari zake.

Nini ugonjwa wa Kifua Kikuu?

Ugonjwa wa kifua kikuu ni wa kuambukiza ambayo yaweza kuleta ugonjwa wa meningitis (kivimbe cha ngozi inayofunika obongo) mionganoni mwa watoto. Vijana na watu wazima kwa jumla, wanaathiriwa katika mapafu yao, lakini yaweza kuathiri vifuko, obongo ama mifupa. Katika nchi hii, watu kwa jumla wanapona kutokana na utabibu, lakini itachukua miezi mingi.

Namna gani ugonjwa wa kifua kikuu unashikwa?

Waweza kushika kifua kikuu kutoka mwagine kama ameshapata ugonjwa huu katika mapafu ama koo, tena anaendelea kukohoa. Wanapokohoa, wanatupilia vitone ambavyo vina vijimea vidogo vidogo. Kama ukivuta vijimea hivyo, utashikwa na ugonjwa huo pia. Ijapokuwa vitone hivi vyaweza kuwepo hewani kwa muda mrefu, lakini kwa jumla itachukua na kuhitaji uhusiano mrefu wa pamoja na mtu mwenye ugonjwa huu kabla haujaenea mionganoni mwa wengine.

Jinsi kifua kikuu inavyoonekana?

Nchini Uingereza, mnamo miaka ya 1950 na baadaye, watu wapatao 50,000 walikuwa wakishikwa na ugonjwa huu kila mwaka. Siku hizi, kiasi hiki kimeshuka hadi kufikia 7,000 ambaao washika ugonjwa huu kila mwaka, lakini kiasi hiki ni bado zaidi ya watu 5,500 wanaoshikwa na kifua kikuu kila mwaka katika miaka ya mwanzoni ya 1990. Basi, inatumainiwa kuwa hutashikwa na ugonjwa huu, watu wote lazima wafahamishwe dalili za kifua kikuu. Jambo hili ni muhimu kwa sababu kifua kikuu kimeenea sana pote duniani. Kutokana na watu wengi wanaosafiri pote duniani siku hizi, hatari ya kushika ugonjwa huu pia imezidi kwa kuwa watu ambaao wameshakaa ama wameshaajiriwa katika nchi za nje watashika ugonjwa huu kutoka wengine ama wataleta ugonjwa huu katika nchi hii.

Dalili nini za kifua kikuu?

Athari za kifua kikuu zitaonekana katika sehemu yo yote ya mwili, basi dalili zake zitakuwa tofauti, na dalili za ugonjwa huu katika mtoto zitatofautiana na zile za mtu mzima. Walakini, kwa kuwa kifua kikuu ni ugonjwa wa kuambukiza, ni muhimu kuwa lazima utambue dalili zake katika mtu mwingine. Inakupasa kuonana na daktari kama mtoto wako, ama ye yote mwingine wa familia yako, ama rafiki yako ana yo yote ya dalili zifuatazo:

- **kikohazi kinachoendelea kwa zaidi ya wiki 3**
- **homa**
- **jasho, hasa katika usiku**
- **kukosa uzito**
- **kujiona uchovu, ama**
- **kukohoa damu**

Kwa nini mtoto wangu anapatiwa dawa la BCG?

Nchini Uingereza, kama nchi nyingi nyingine, dawa la BCG linatolewa kwa watoto ambao waweza kushika haraka ugonjwa wa kifua kikuu kuliko watu wengine wanaohusika na watu wenyewe maradhi hii. Kwa sababu hao wanakaa katika sehemu zenyeye hali ya kuvuta ugonjwa huu ama wazazi wao ama mababu wao walihamia kutoka nchi zinazopata ugonjwa huo. Kwa jumla inamaanisha kuwa watoto wanaoishi katika sehemu za katikati za mijini. Dawa hili linatolewa kwa watoto mara baada ya kuzaliwa wakati mtoto bado katika hospitali, lakini dawa hili laweza kutolewa hata baadaye pia.

Jinsi mtoto wangu atajihifadhi kutokana na ugonjwa?

Mtoto wako atatolewa dawa la BCG kuitia sindano kwenye sehemu ya juu ya mkono wa kushoto.

Je, ziko athari zo zote za chanjo?

Mara baada ya chanjo, lengelenge litaonekana. Inamaanisha kuwa chanjo limefanikiwa.

Mnamo wiki 2 hadi 6 tangu kuchanjwa, nishani ndogo itaonekana. Itakuwa ya kuwasha kwa siku chache, lakini itapona polepole kama hufuniki. Baada ya kupona, kovu ndogo itabaki.

Mara nyingi, watoto kadha watakuwa na kidonda kidogo pale walipochanjwa. Kama maji inatoka na kuhitaji kufunikwa, tumia kitambaa kikavu – lakini usitumie lipu hata kidogo – mpaka kigaga kisipotokea. Kidonda hiki kitachukua miezi mingi ya kupona.

Kama una wasiwasi ama unafikiri kidonda hiki kimeambukizwa, mgusie daktari yako.

Je, sababu yo yote kuwa mtoto wangu asichanjwe dawa la BCG?

Kwa vile ilivyo katika machanjo mengine, mtoto asichanjwe ama kuahirishwa ikiwa mtoto wako:

- mtoto ana homa nyingi
- mtoto ana utabibu wa cancer (kensa) ama ugonjwa mwingine mbaya unaodhoofisha mwili
- ana ugonjwa wa AIDS ama
- ana ugonjwa wa ngozi, kwa vile wa upele mbaya.

Je, nahitaji kujua mambo yo yote mengine?

Mtoto wakoaweza kuchanjwa dhidi ya maradhi mengine kama zile za diphtheria, tetanus, kifaduro, polio, Haemophilus influenzae ya aina ya b (Hib) na ngozi inayofunika obongo C wakati umri wake ni miezi 2 bila ya kujali kama anachanjwa kwa ugonjwa wa kifua kikuu.

Walakini, lazima hakikisha kuwa mtoto wako asichanjwe yo yote katika mkono alipochanjwa kwa ugonjwa wa kifua kikuu wa BCG kwa muda wa miezi 3, ama sivyo sehemu kadha za ngozi zitavimba.

Pia hakikisha kwamba habari ya kuchanjwa kwa dawa la BCG imetajwa katika kijitabu cha bi nafasi cha afya ya mtoto (Personal Child Health Record) (PCHR) kwa ajili ya kuhakikishia hapo baadaye.

Nchi ambapo ugonjwa wa kifua kikuu unaonekana kwa wingi

Nchi zilizotajwa hapo chini zina kesi nyingi za kifua kikuu. Kama unajibu ‘**NDIYO**’ kwa swali yo yote, mtoto wako lazima achanjwe kwa dawa la BCG kama hakuchanjwa hapo awali:

- Wewe, familia yako ama baba wa mtoto ama familia yake anatoka mojawapo ya nchi hizo?
- Wewe ama mtoto wako anashauri ya kukaa katika nchi hiyo kwa zaidi ya mwezi mmoja ama kusafiri kwa muda mrefu katika siku zijazo?
- Je, yuko ye yote katika nyumba yako ama mwingine atakayehusika na mtoto wako, aliyekuwa na ugonjwa wa kifua kikuu hapo awali ama anatoka nchi yo yote kati ya nchi hizo?

9

Afghanistan		
Albania	Côte d'Ivoire	-----
Algeria	Croatia	Kazakhstan
American Samoa	-----	Kenya
Angola	Democratic People's	Kiribati
Argentina	Republic of Korea	Kuwait
Armenia	Democratic People's	Kyrgyzstan
Azerbaijan	Republic of Congo	Korea
-----	Djibouti	-----
Bahamas	Dominican Republic	Lao People's
Bahrain	-----	Democratic
Bangladesh	Ecuador	Republic
Belarus	El Salvador	Latvia
Belize	Equatorial Guinea	Lesotho
Benin	Eritrea	Liberia
Bhutan	Estonia	Lithuania
Bolivia	Ethiopia	-----
Bosnia Herzegovina	-----	Macedonia
Botswana	Gabon	Madagascar
Brazil	Gambia	Malawi
Brunei Darussalam	Georgia	Malaysia
Burma (Myanmar)	Ghana	Mali
Bulgaria	Guam	Marshall Islands
Burkina Faso	Guatemala	Mauritania
Burundi	Guinea	Mauritius
-----	Guinea-Bissau	Mexico
Cambodia	Guyana	Micronesia
Cameroon	-----	(Federated
Cape Verde	Haiti	States of)
Central African Republic	Honduras	Moldova
Chad	-----	Mongolia
China	India	Morocco
Colombia	Indonesia	Mozambique
Comoros	Iraq	Myanmar
Congo	-----	
Cook Islands	Japan	

10		
Namibia	Timor-Leste	
Nepal	Toga	
New Caledonia	Tokelau	
Nicaragua	Tonga	
Niger	Turkey	
Nigeria	Turkmenistan	
Northern Mariana Islands	Tuvalu	
<hr/>		
Pakistan	Uganda	
Palau	Ukraine	
Panama	United Republic of Tanzania	
Papua New Guinea	Uzbekistan	
Paraguay	<hr/>	
Peru	Vanuatu	
Philippines	Venezuela	
<hr/>		
Qatar	Viet Nam	
<hr/>		
Republic of Korea	Yemen	
Republic of Moldova	Zambia	
Romania	Zimbabwe	
Russian Federation		
Rwanda		
<hr/>		
Samoa		
Sao Tome and Principe		
Saudi Arabia		
Senegal		
Serbia & Montenegro,		
Seychelles		
Sierra Leone		
Singapore		
Solomon Islands		
Somalia		
South Africa		
Sri Lanka		
Sudan		
Suriname		
Swaziland		
Syrian Arab Republic		
<hr/>		
Tajikistan		
Tanzania		
Thailand		

Kumbuka, utabibu wa ugonjwa wa TB unachukua muda mrefu, uzuiji wake ni rahisi sana.

Simu ya NHS Direct 0845 46 47

Habari Zaidi

Kwa habari zaidi juu ya kujihifadhi, familia na marafiki kutokana na kifua kikuu, unaweza kuulizia:

- NHS Wales Direct kwa simu namba 0845 46 47
- Daktari wako **ama**
- TB Alert, shirika linalotoa habari zote juu ya ugonjwa huu na kukabiliana na dalili zake pote duniani

Shirika la TB Alert linaweza kupatikana kwenye:

22 Tiverton Road
London
NW10 3HL
Simu: 0845 456 0995
e-mail: info@tbalert.org
Reg Charity No: 1071886

Unaweza kujipatia habari kutoka mitandao ifuatayo:

www.who.int
www.hpa.org.uk
www.tbalert.org
www.dh.gov.uk
www.immunisation.nhs.uk

Huduma za kiutendaji za NHS Wales Direct Interactive zinatoa habari za kawaida za afya kupitia mkondo wa Television wa aina maalum kwa kutumia ufunguo wa kiutendaji katika chombo cha television.

Ukurasa huu unapatikana kutoka kwa Mganga Mkuu wa Wales kwenye Mtandao wa:

<http://www.cmo.wales.gov.uk/content/work/immunisation/index-e.htm>

katika lugha zifuazo:

KIARABU	KIPUNJABI
KIBULGARIAN	KIPOLISH
KIBENGALI	KIRENO
KICZECH	KIRUSSI
KIPSPANIA	KISOMALI
KIFARSI	KISWAHILI
KIFARANSA	KITAGALOG
KIGUJARATI	KIURDU
KIHINDI	KIVIETNAMESE
KIKURDISH (KISORANI)	KICHINA
KILINGALA	

Nakala zake zinaweza kupatikana kutoka mitando inayohusika ama kuombwa kutoka ofisi za Baraza la Kutunga Sheria:

Public Health Protection Division,
Welsh Assembly Government
Cathays Park, Cardiff CF10 3NQ

Anwani nyingine:

E-mail: jenny.thorne@wales.gsi.gov.uk
Simu: Neil Robins 029 2082 5397 ama
Matthew Thomas 029 2082 5410

© Crown Copyright Juni 2005
Jarida la Idara ya Afya (Department of Health publication)
Kielelezo: Serikali ya Baraza la Wales



Llywodraeth Cymru
Welsh Assembly Government

SW - SWAHILI